

**MKUTANO WA SHIRIKA LA KAZI LA UMOJA WA MATAIFA**

**MAKUBALIANO YA KIMATAIFA JUU YA WATU WA ASILI NA  
MAKABILA KATIKA NCHI HURU.**

**MAKUBALIANO**

**MKUTANO WA SHIRIKA LA KAZI LA UMOJA WA MATAIFA.  
MAKUBALIANO YA KIMATAIFA JUU YA WATU WA ASILI NA MAKABILA  
KATIKA NCHE HURU.**

**MAKUBALIANO NAMBA 169.**

Baada ya Mkutano wa kawaida wa Shirika la Kazi la Umoja wa Mataifa kukutana Geneva kwenye ofisi za shirika hilo, na baada ya kukutana katika kikao chao cha 76 mnamo tarehe 7 June 1987 na:

Kwa kutambua hali za kimataifa zilizopendekezwa na mkutano wa jumuiya za asili na makabila wa 1957, na

Kwa kuitikia masharti yaliyowekwa na Azimio la haki za binadamu la Umoja wa Mataifa, Mkataba wa Kimataifa wa haki za Kiuchumi, Kijamii na Kijutamaduni. Mkataba wa kimataifa uhusu haki za Kibinadamu za kisiasa, na vyombo vingine vingi kuhusu uzuiji wa ubaguzi, na

Kufikiria kwamba maendeleo yaliyoletwa na sheria za kimataifa tangu 1957 pamoja na maendeleo katika hali ya watu wa asili; na makabila katika pande zote za dunia imepelekea haja ya kupitisha vipimo vipya vya kimataifa kwa madhumuni ya kufutilia mbali ile hali ya mfumo uliokuwepo katika hali iliyokuwepo hapo awali na hivyo kulazimishia kuwepo mfumo wa kuwabagua watu wengine.

Kutambua ile ari ya watu wa asili kuhitaji madaraka juu ya taasisi zao wenyewe, mienendo ya maisha yao na maendeleo yao ya kiuchumi, pamoja na kudumisha na kuendeleza utu wao, lugha na dini ndani ya mfumo ya nchi wanamoishi.

Kwa kutambua kwamba sehemu nyingi duniani watu wa asili wameshindwa kufaidi haki zao za msingi kwa kiwango kile kile cha watu wengine ndani ya nchi wanamoishi, na kwamba sheria zao, matakwa yao, desturi zao na hata mitazamo yao imekuwa ikimomonyolewa, na

Ikitaliwa maanani na kuonekana wazi kuwa michango mbalimbali ya watu wa asili na makabila katika nyanja za usambaaji wa tamaduni na uwiano wa uhai wa jamii za kibinadamu na ushirikiano na uelewano wa kimataifa ni mkubwa, kutambua vile vile kwamba tathmini yote hii imefanywa kwa ushirikiano wa Umoja wa Mataifa, Shirika la Kilimo na Chakula duniani la Umoja wa Mataifa, Shirika la Elimu Sayansi na Utamaduni, Shirika la Afya duniani, pamoja na Taasisi ya pamoja ya Kimarekani na Kihindi katika ngazi mbali mbali katika nyanja zilizohusika, na kwamba inapendekwa kuendeleza ushirikiano huu katika kukuza na kulinda matumizi tathmini hii.

Baada ya kamua kupitisha baadhi ya mapendekezo yahasuyo urekebishaji wa mkutano wa watu wa asili na makabila, 1957 (No. 107) ambayo ni agenda ya nne katika kikao hiki, na

Baada ya kuzingatia kwamba mapendekezo haya yatachukuwa sura ya makubaliano ya Kimataifa unaorekebisha mkataba wa Kimataifa wa watu wa Asili na makabila 1957.,

Hivyo unapitisha makubaliano yafuatayo leo tarehe 27/6/1989 ambayo yatajulikana kama makubaliano ya watu wa asili na makabila 1989.

## SEHEMU YA KWANZA – SERA YA JUMLA

### IBARA YA 1

1. Makubaliano yatafanya kazi kwa:-
  - a). Makebila katika nchi huru ambao hali zao za kijamii, kiutamaduni na kiuchumi huwatofautisha na sehemu nyingine za jamii ya kitaifa na ambazo hadhi yao inatawaliwa moja kwa moja na mila au desturi zao wenyewe au kwa sheria maalum au taratibu.
  - b). Watu katika nchi huru ambao hutambuliwa kama watu wa asili kwa vile ni vizazi vya jumua zilizowahi kuishi hapo au katika ukanda fulani Kijiografia ambao nchi hiyo ipo, wakati wa uvamizi au ukoloni, au urwekaji wa mipaka ya nchi iliyopo hata sasa na ambao bila kujali hadhi yao kisberia bado wanashikilia taasisi zao za kijamii, kiuchumi, kiutamaduni na kisiasa kwa kiasi fulani au kwa ujumla.
2. Kujitambua binafsi kuwa wa asili au kabila kutachukuliwa kama kigezo cha msingi cha kutambua vikundi ambavyo ibara za makubaliano haya zitahusu.
3. Matumizi ya dhana "WATU" katika makubaliano haya hayatamaanisha kwamba yana ngongano wowote na haki ambazo zimefungamana na dhana hiyo katika sheria ya Kimataifa.

### IBARA YA 2

1. Serikali zitawajibika kwa ushirikiano na wahusika, kuendeleza na kuratibu mikakati ya kulinda haki za watu hawa na kuwahakikishia heshima ya utu wao.
2. Mikakati hiyo itajumuisha hatua za:-
  - a). Kuhakikisha kwamba kila mmoja wao anafaidi kwa kiasi kile kile haki na nafasi ambazo zimetolwa na sheria na taratibu kwa wakazi wengine.
  - b). Kuhimiza kutambuliwa kwa haki zao kiuchumi na kiutamaduni kwa kuheshimu hali yao ya kijamii na kiuchumi, mila zao, desturi zao na taasisi zao.
  - c). Kuwasaidia watu wa jumua zinazohusika kufutilia mbali tofauti za kijamii na kiuchumi zilizopo kati ya watu wa asili na watu wengine wa jamii katika taifa husika, kwa namna inayokubaliana na dhamira zao na njia zao za kuishi.

**IBARA YA 3**

1. Watu wa asili na makabila watafaidi kikamilifu haki zote za binadamu na uhuru wa kimsingi bila kizuizi wala ubaguzi. Ibara za makubaliano haya zitatumika bila ubaguzi kwa wanaume wala wanawake wa watu hawa.
2. Aina yoyote ya nguvu au vishawishi haitatumika kukiuka haki za binadamu na uhuru wa kimsingi wa watu wanaohusika ikiwa ni pamoja na haki zilizomo kwenye makubaliano haya.

**IBARA YA 4**

1. Hatua maalum zitatumika ipasavyo kwa kuwafinda watu, taasisi, mali, kazi, mila na mazingira ya jumua zinazohusika.
2. Hatua hizo maalum hazitakuwa kinyume na maoni huru na mategemeo ya wahusika.
3. Haki za kufaidi uraia bila ubaguzi hazitaingiliwa kwa njia yoyote na hatua hizo maalum.

**IBARA YA 5**

Katika matumizi ya Ibara za makubaliano haya:-

- a). Mitazamo ya watu hawa ya kijamii, kiutamaduni, kidini na kiroho itatambuliwa na kufindwa na viini vya matatizo yanayowakabili kama vikundi au watu binafsi vitachunguzwa.
- b). Hadhi ya mitazamo, matendo na taasisi za watu hawa zitaheshimiwa.
- c). Sera zinazolenga kupunguza matatizo waliyoyapata watu hawa katika kukabiliana na mazingira mapya ya maisha na kazi, zitapokelewa kwa kuwahusisha watu walioathiriwa.

**IBARA YA 6**

Katika matumizi ya Ibara hizi serikali zita:-

1.
  - a). Wasiliana na wahusika kupitia taratibu zinazohusika hasa kupitia taasisi zinazowawakilisha, pale inapofikiwa kutunga sheria au kufanya tendo lolote la kiutawala au la kisheria linalowaathiri moja kwa moja.
  - b). Anzisha namna ambazo kwazo watu hawa wanaweza kushiriki kwa hiari walau kwa kiwango kile kile cha sekta zingine za jumua, katika ngazi zote za umuzi katika taasisi chaguzi na za kiutawala na vyombo vingine vyote vyenye mamlaka na sera na mipango inayowahusu.
  - c). Anzisha namna ya maendeleo kamili ya taasisi na mipango ya watu hawa na pale inapobidi kutoa vifaa vinavyotakiwa kwa ajili hiyo.
2. Mashauriano yaliyofanyika kwa kutekeleza makubaliano haya, yatatumika

kwa nia njema na katika hali inayokubalika kwenye mazingira yanayohusika kwa madhumuni ya kufikia makubaliano au idhini kwa hatua zilizopendekezwa.

### **IBARA YA 7**

1. Watu wahusika watakuwa na haki ya kujiamulia vipaumbele vyao wenyewe katika harakati za maendeleo kama yanavyoathiri masiha yao, imani, taasisi na ubora wao kiroho na nchi wanamoishi au kivingine wanayoitumia na kuwa na madaraka kwa kiasi kiwezekanacho juu ya maendeleo yao kiuchumi, kijamii na kiutamaduni.  
Zaidi ya hayo watashiriki katika kubuni, kutekeleza na kutathmini mipango ya miradi ya maendeleo ya kitaifa na kikanda ambayo yaweza kuwaathiri moja kwa moja.
2. Uboreshaji wa hali ya maisha na ya kikazi na ngazi za afya na elimu kwa wahusika pamoja na kushiriki kwao na ushirikiano wao litakuwa ni swala la kipaumbele katika mipango ya jumla ya kiuchumi kwenye maeneo wanayoyakalia. Miradi maalum kwa maendeleo ya maeneo yanayohusika pia yatafangiliwa ili kuleta ubora huo.
3. Serikali zitahakikisha kwamba, pale inapofaa utafiti unafanyika kwa ushirikiano na wahusika kutathmini jinsi walivyoathirika kijamii kiroho, kitaaluma na kimazingira katika mikakati yao na maendeleo. Matokeo ya utafiti huu yatachukuliwa kama kigezo cha utekelezaji wa shughuli hizi
4. Serikali zitachukuwa hatua, kwa ushirikiano na wahusika, kulinda na kuhifadhi mazingira ya maeneo wanayoishi.

### **IBARA YA 8**

1. Katika kutekeleza sheria za kitaifa na taratibu kwa watu hawa, desturi na sheria zao za kimita zitazingatiwa.
2. Watu hawa watakuwa na haki ya kubakia na desturi zao wenyewe na taasisi pale ambapo havijiugani na mfumo wa sheria wa kitaifa pamoja na haki za binadamu zinazotambulika kimataifa. Taratibu zitaanzishwa pale itakapofaa kusufuhisha mgongano itakayojitokeza kutokana na matumizi ya haki hii.
3. Matumizi ya aya 1 na 2 za Ibara hii hayatawazuia watu hawa kutumia haki zile zilizotolewa kwa raia wote na kuchukua majukumu yatakanayo.

### **IBARA YA 9**

1. Kwa kiwango kinachokubaliana na mfumo wa kisheria wa kitaifa na haki za binadamu zinazotambulika kimataifa, njia zao za kidesturi zinazotumika kupambana na makosa ya jinai yaliyofanywa wa watu wa jamii hizo zitaheshimiwa.
2. Desturi za watu hawa zihusianazo na maswala ya adhabu zitatiliwa maanani na mamlaka na mahakama zinazoshughulikia mashauri yanayohusika.

**IBARA YA 10**

1. Wakati wa kutoa adhabu zilizopo kwenye sheria ya kawaida kwa watu hawa, hali zao za kijamii na kimila zitakurwa kigezo kikuu.
2. Uzito utawekwa kwa njia nyingine za adhabu kuliko kufungwa jela (gerezani).

**IBARA YA 11**

Ulazimishaji kwa watu hawa kwenye shughuli za lazima, kwa malipo au bila malipo utapigwa marufuku na kuadhibiwa kisheria isipokuwa tu maswala yaliyockwa kisheria kwa raia wote.

**IBARA YA 12**

Wahusika watalindwa dhidi ya ukukwaji wa haki zao na watakuwa na uwezo wa kuchukuwa hatua za kisheria, kwa mtu binafsi au kupitia vyombo vyao vinavyowawakilisha kudai ulinzi kamili wa haki hizi. Hatua zitachukuliwa kuhakikisha kwamba watu hawa wanaweza kuelewa na kueleweka katika shughuli za kimahakama (kisheria) pale inapobidi kwa kutafsiriwa au kwa njia nyingine zinazofaa.

**SEHEMU YA PILI – ARDHI****IBARA YA 13**

1. Katika kutumia Ibara ya sehemu hii ya makubaliano, serikali zitatilia umuhimu utamaduni na mitazamo ya kiroho ya wahusika pamoja na uhusiano baina yao na ardhi au maeneo, wanayomiliki au kutumia hasa miantarafu ya pamoja ya uhusiano huu.
2. Matumizi ya neno "Ardhi" katika Ibara ya 15 na 16 yatajumisha maeneo yanayochukuwa mazingira yote kwa ujumla ya sehemu ambazo wahusika wanakalia au kutumia.

**IBARA YA 14**

1. Haki za umilikaji na utwaaji kwa watu hawa juu ya ardhi wanazozikalia kimila zitatambuliwa. Zaidi ya hayo hatua zitachukuliwa katika mashauri yanayofaa katika kulinda haki za wahusika za kutumia ardhi ambayo hawaikalii peke yao bali wana haki nayo kimila kwa ajili ya kukidhi maisha yao na shughuli za kiotamaduni. Watu wenye asili ya kuhamahama ndio hasa watakaotiliwa mkazo kwa ajili hii.
2. Serikali zitachukuwa hatua muhimu kutambua ardhi ambayo wahusika wanazikalia kimila na kuhakikisha ulinzi kamili wa haki zao za umilikaji na utwaaji.
3. Taratibu zinazofaa zitaanzishwa ndani ya mfumo wa sheria kitaifa kutatua madai ya ardhi ya wahusika.

## IBARA YA 15

1. Haki za wahusika kwa mali asili zitokanazo na ardhi zao zitalindwa mahsusi. Haki hizi zinajumuisha haki ya wahusika kushiriki matumizi, uendeshaji na ulifadhi wa mali asili hizo.
2. Pale ambapo serikali (dola) imejitwalia umilikaji wa madini au majiasili zinazopakana karibu na uso wa ardhi haki zingine, zinazotokana na ardhi yao, serikali zitaanzisha na kudumisha taratibu zitakazotumika kuwasiliana na watu hawa kwa nia ya kuhakikisha ni kwa kiwango gani manufaa yao yataathirika kabla ya kuchukuwa jukumu au kuruhusu mipango yoyote ya kutafuta au kuchimba (kuvuna) majiasili hizo ziambatanazo na ardhi yao. Watu wahusika kila inapowezekana watahiriki faida ya shughuli hizo na watapatiwa fidia halali kwa madhara yanayoweza kupata kama matokeo ya shughuli hizo.

## IBARA YA 16

1. Bila kuathiri ya zifuatazo za Ibara hii, wahusika hawataondolewa kwenye ardhi wanazozikalia.
2. Ikiwa kuhamishwa watu hawa kumeonekana lazima kama hatua ya pekee, uhamisho huo utafanyika tu kwa taarifa na ridhaa isiyo na shinikizo kwa watu hawa. Pale ridhaa yao isipoweza kupatikana uhamisho utafanyika kufuatilia taratibu zinazokubalika zilizosimikwa na sheria na taratibu za kitaifa zinazotoa fursa ya uwakilishi halisi wa wahusika ikiwa ni pamoja na kura ya maoni ikibidi.
3. Pale inapowezekana, watu hawa watakuwa na haki kurudi kwenye ardhi zao za kijadi mara sababu za uhamisho huo zinapokuwa hazipo tena.
4. Ikiwa kurudi kwao hakuwezekani kama ilivyoamuliwa kwa makubaliano, au bila makubaliano hayo, kupitia taratibu zilizokubalika, watu hawa kwa hali zote zinazowezekana, watapewa ardhi yenye thamani na hadhi ya kisheria watau karibu sawa na ile waliyokalia, inayofaa kuwapatia mahitaji yao kwa wakati huo na maendeleo ya baadaye. Pale wahusika watakapodhibirika kupendelea fidia ya fedha au mali, watafidiwa hivyo kwa uthibitisho unaokubalika.
5. Watu waliohamishwa watafidiwa kikamilifu kwa hasara au madhara yatokanayo.

## IBARA YA 17

1. Taratibu zilizowekwa na wahusika za ubadilishanaji haki za ardhi baina yao zitaheshimiwa.
2. Maoni yawahusika yatatafutwa pale ambapo inafikiriwa kuchukua ardhi yao au vinginevyo kupeleka haki yao sehemu nyingine nje ya jamii yao.
3. Watu wasio na asili ya watu hawa watazuiliwa kujinufaisha na desturi zao au kujitwalia umilikaji, ukabaji au matumizi ya ardhi zao kwa kigezo cha wao kutoelewa sheria zinazowahusu.

**IBARA YA 18**

Adhabu inayostahili itawekwa kisheria kwa uingiliaji kiholela wa matumizi ya ardhi za wahusika na serikali itachukuwa hatua kuzuia uhalifu wa aina hii.

**IBARA YA 19**

Mipango ya kilimo ya kitaifa itatoa nafasi sawa kwa watu hawa kama ile iliyotolewa katika jamii nyingine za wakazi kuhusu:-

- a). Kutoa ardhi zaidi kwa watu hawa wanapokosa enco lifaalo kuwapatia mabitaji muhimu ya maisha ya kawaida au kwa uwezekano wa ongezeko la idadi yao.
- b). Kuwapatia jinsi inavyohitajika kukuza maendeleo ya ardhi ambazo watu hawa wanazo tayari.

**SEHEMU YA TATU – AJIRA NA MASHARTI YA AJIRA  
IBARA YA 20**

1. Ndani ya mfumo wa sheria za nchi na taratibu na kwa ushirikiano na wahusika, Serikali zitachukuwa hatua madhubuti zitakazolinda ajira na masharti ya ajira kwa watu hawa pale ambapo hawafindwi na sheria sawa na wafanyakazi kwa wengine.
2. Serikali zitafanya kila hwezekanalo kuzuia ubaguzi baina ya wafanyakazi watokanao na wahusika na wafanyakazi wengine ikizingatia:-
  - a). Kupokelewa kazini ikiwa ni pamoja na kazi za ujuzi pamoja na hatua za kupandishwa vyeo na kujiendeleza.
  - b). Mishahara sawa kwa kazi zenye umuhimu sawa.
  - c). Misaada ya kiafya na kijamii, usalama kazini na afya, manufaa ya uzeeni na marupurupu yote yahusikanayo kikazi na nyumba.
  - d). Haki ya kuwasitiana na uhuru wa shughuli za vyama vya wafanyakazi na hali ya kufikia maamuzi ya pamoja na waajiri au taasisi zawaajiri.
3. Hatua zitakazochukuliwa zitajumuisha kuhakikisha kwamba:-
  - a). Wafanyakazi wanaotokana na wahusika kujumuisha wale wa msimu, vibarua na wahamiaji katika kilimo na ajira nyingine, pamoja na wale walioajiriwa na makandarasi wanafaidi bifaadhi iliyotolewa na sheria ya taifa kwa wafanyakazi wengine wa sekta za aina hiyo na kwamba wana taarifa ya haki zao chini ya sheria za kazi na njia za utetezi zilizopo kwa ajili yao.
  - b). Kwamba wafanyakazi watokanao na wahusika hawapewi masharti ya kazi hatari kwa afya zao hasa yale ya dawa za kuuwa wadudu na madawa mengine ya sumu.
  - c). Kwamba wafanyakazi watokanao na wahusika hawataingizwa kwenye ajira za kulazimishwa ikiwa ni pamoja na kazi za kiutumwa na aina zote za mtu kuwa

mtunwa wa madeni.

d). Kwamba wafanyakazi watokanao na wahusika wanafaidi nafasi sawa katika ajira waume kwa wako na wanalindwa dhidi ya unyanyasaji wa kijinsia.

4. Mkazo utawekwa wa kuanzisha huduma za ukaguaji wa kazi kwenye maeneo ambayo watu watokanao na wahusika wanafanya kazi za ujira ili kuhakikisha utekelezaji wa sehemu hii ya mkutano huu.

## **SEHEMU YA NNE - MAFUNZO YA UFUNDI KAZI ZA MIKONO NA VIWANDA VYA VIJINI**

### **IBARA YA 21**

Wahusika watafaidi fursa sawa na zile za raia wengine katika mafunzo ya ufundi.

### **IBARA YA 22**

1. Hatua zitachukuliwa kukuza kushiriki kwa hiari kwa wahusika katika mipango ya mafunzo ya ufundi unaotakikana zaidi.
2. Endapo mipango iliyopo ya mafunzo ya ufundi wa kawaida haikidhi mahitaji ya wahusika, serikali, kwa kuwashirikisha watu hawa, zitahakikisha upatikanaji wa mafunzo maalum na vifaa.
3. Mipango ya mafunzo maalum itashikilia mazingira ya kiuchumi, haki ya kijamii na kiutamaduni na mahitaji ya kimsingi ya wahusika. Utafiti wowote utakaofanyika kwa watu hawa utakuwa kwa ushirikiano wao ambapo wataarifiwa kuhusu mipango na utekelezaji wake. Pale utafiti utakapokubalika, watu hawa watachukuwa madaraka ya mipango na utekelezaji wa mafunzo hayo kama wakiamua.

### **IBARA YA 23**

1. Kazi za mikono, viwanda vilivyo mikononi mwa vijiji au jumuiia na uchumi wa kujikimu wa wahusika kama uwindaji, uvuvi, utegaji na ukusanyaji vitatambuliwa kama vigezo muhimu vya kukuza mila zao na pia katika kujitegemea kiuchumi na kimaendeleo. Serikali kwa ushirikiano na watu hawa na kila inapobidi zitahakikisha kwamba shughuli hizi zinakaziwa na kukuzwa.
2. Kwa maombi kutoka kwa wahusika, msaada unaofaa wa kiufundi na kifedha utatolewa panapokuwa na uwczekano ikichuliwa maanani taaluma za kijadi na tabia za kimila za watu hawa pamoja na umuhimu wa maendeleo yanayoonekana na kufaa.

## SEHEMU YA TANO - USALAMA WA KIJAMII NA WA KIAFYA

### IBARA YA 24

Mipango ya usalama wa kijamii itasambazwa kuwafikia wahusika na itatekelezwa bila ubaguzi dhidi yao.

### IBARA YA 25

1. Serikali zitahakikisha kwamba huduma za kiafya zinazofaa zinapatikana kwa wahusika au zitawapatia vifaa kuwawezesha kuunda na kutoa huduma hizo chini ya mamfaka na udhibiti wao wenyewe ili waweze kufaidika kwa kiwango cha juu zaidi kwa afya kimwili na kiakili.
2. Huduma za afya kwa kiwango kinachowezekana zitakuwa mikononi mwa jamii. Huduma hizi zitapangwa na kuendeshwa kwa ushirikiano na wahusika na kutilia maanani haki zao, kiuchumi, kijiografia, kijamii na kiutamaduni pamoja na kinga zao za kijadi, tiba na dawa.
3. Mfumo wa afya utatoa kipaumbele kwa mafunzo na ajira ya wafanyakazi wa afya kutoka katika jamii hizi na kuangalia afya ya msingi ikiunganishwa kikamilifu na ngazi zingine za huduma ya afya.
4. Utoaji wa huduma hizo za afya zitaratibiwa pamoja na shughuli zingine za kijamii, kiuchumi na kijadi katika nchi.

## SEHEMU YA SITA - ELIMU NA NJIA ZA MAWASILIANO

### IBARA YA 26

Hatua zitachukuliwa kuhakikisha kwamba wahusika watapata nafasi sawa ya kupata elimu katika ngazi zote walau kwa kiwango sawa na jumua nyingine ya kitaifa.

### IBARA YA 27

1. Mipango ya elimu na huduma kwa wahusika itacendelezwa na kutekelezwa kwa ushirikiano nao kukidhi haja zao maalum na itajumuisha historia zao, ujuzi wa taaluma, mifano ya mitazamo yao, na maendeleo ya ari zao kijamii, kiuchumi na kijadi.
2. Mamfaka yenye uwazo itahakikisha mafunzo kwa watu hawa na kujihusisha kwao kwenye kubuni na kutekeleza mipango ya elimu kwa ajili ya kuhamishia wajibu wa uendeshaji wa mipango hii kwao kwa namna inavyohitajika.
3. Zaidi ya hayo, Serikali zitatambua haki za watu hawa kuanzisha taasisi zao wenyewe za elimu na huduma ili miradi zinakidhi kiwango kilichowekwa na mamfaka yenye wajibu huo kwa kuwasiliana na watu hawa. Vifaa vinavyohitajika vitatolewa kwa ajili hii.

**IBARA YA 28**

1. Watoto wanaotoka katika jamii hizi, pale inapowezekana, watafundishwa kusoma na kuandika kwa lugha yao ya asili au kwa lugha rasmi ya kundi au jamii wanafotoka, pale ambapo hili haliwezekani, mamlaka husika itapokea ustauri kutoka kwa watu hawa kwa lengo la kuunda utaratibu wa kufikia nia hii.
2. Hatua zinazofaa zitachukuliwa kuhakikisha kwamba watu hawa wanayo nafasi (fursa) ya kuifahamu fika lugha ya taifa au moja wapo ya lugha rasmi za nchi.
3. Hatua zitachukuliwa kuhifadhi na kukuza maendeleo na matumizi ya lugha asili za wahusika.

**IBARA YA 29**

Kutoa elimu ya jumla na maarifa yatakayowasaidia watoto wa wahusika kushirikiana kikamilifu na kwa hali sawa katika jumuiya yao wenyewe na katika taifa, litakuwa ndilo lengo la elimu kwa watu hawa.

**IBARA YA 30**

1. Serikali zitachukuwa hatua zinazokubaliwa na jadi na mila za wahusika kuwajulisha haki na majukumu yao hasa kuhusiana na kazi, nafasi yao ya kiuchumi, elimu na mambo ya afya, ustawi wa jamii na haki zao zitokanazo na makubaliano haya.
2. Ikibidi hii itafanyika kwa kutumia tafsiri za kimaandishi na kupitia mawasiliano ya umma kwa lugha zao wenyewe.

**IBARA YA 31**

Hatua za kielimu zitachukuliwa miongoni mwa sehemu zote za jumuiya ya taifa na hasa miongoni mwa wale ambao wana mawasiliano ya karibu na wahusika kwa nia ya kufutia mbali mawazo potofu au kasumba yanayoweza kujitokeza juu ya watu hawa. Ili kufikia hilo juhudi zitafanyika kuhakikisha kwamba vitabu vya kiada vya historia na vifaa vingine vya elimu vinatoa picha na habari halisi na sahihi za jamii na tamaduni za watu hawa.

**SEHEMU YA SABA - MAWASILIANO NA USHIRIKIANO NG'AMBO YA MIPAKA****IBARA YA 32**

Serikali zitachukuwa hatua zifaazo, ikiwa ni pamoja na kutuma mikataba ya kimataifa kuwezesha ushirikiano pana ya watu wa asili ng'ambo ya mipaka, ikijumuisa shughuli katika nyanja za kiuchumi, kijamii, kijadi, kiroho na kimazingira.

**SEHEMU YA NANE – UTAWALA****IBARA YA 33**

1. Mamlaka za kiserikali zenye wajibu wa mambo yaliyopitiwa na makubaliano haya yatahakikisha kwamba vyombo au mifumo inayofaa ipo kusimamia mipango inayowaathiri wahusika na zitahakikisha kwamba zina ryezo muhimu kwa ufanikishaji halisi wa majukumu waliyokabidhiwa.
2. Mipango hii itajumuisha:-
  - a). Kupanga, kuhamasisha, kutekeleza na kutathmini, kwa ushirikiano na wahusika, hatua zilizotolewa ndani ya makubaliano haya.
  - b). Kupendekeza hatua za kisheria na zinginezo kwa mamlaka zinazowajibika na kusimamia matumizi ya hatua zilizo chukuliwa kwa ushirikiano na wahusika.

**SEHEMU YA TISA: VIFUNGU VYA JUMLA****IBARA YA 34**

Chimbuko na upana wa vipimo vitakavyotunika kutekeleza sheria hii vitatumika kwa utaratibu unaotofautiana kulingana na mazingira na tabia ya kila nchi.

**IBARA YA 35**

Utekelezaji wa vifungu vya sheria hii havitaathiri haki na nafuu ya watu wanaohusika kwa kuzingatia sheria zingine, mapendekezo, mikataba, sheria za nchi, taratibu na mila na makubaliano.

**SEHEMU YA KUMI - VIFUNGU VYA MWISHO****IBARA YA 36**

Makubaliano haya yanabadilisha Makubaliano ya awali ya Shirika la Kazi la Umoja wa Mataifa juu ya Watu wa Asili na Makabila ya mwaka 1957.

**IBARA YA 37**

Maridhio rasmi ya makubaliano haya, yatawasilishwa kwenye ofisi ya Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kazi Duniani kwa ajili ya kuandikishwa.

**IBARA YA 38**

1. Makubaliano haya yatawabana tu wale wanachama wa Shirika la Kazi la Umoja wa Mataifa ambao wameandikisha maridhiano ya makubaliano haya kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kazi Duniani.
2. Yataanza kutumika miezi 12 tangu wajumbe wawili walipoandikisha kuridhia kwao Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kazi Duniani.

3. Baada ya hapo, makubaliano haya yataanza kutumika kwa mjumbe mmoja mmoja miezi 12 tangu mjumbe huyo alipoandikisha maridhiano.

#### **IBARA YA 39**

1. Mjumbe aliyeridhia makubaliano haya, anaweza kujitoa baada ya miaka kumi kupita tangu makubaliano haya yalipoanza kutumika kwa kutoa mawasiliano kwa Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kazi duniani, Kujitoa huko hakutatambuliwa mpaka baada ya mwaka mmoja tangu ajiandikishe.
2. Kila mwanachama aliyeridhia makubaliano na kuandikishwa na ambaye katika kipindi cha mwaka mmoja tangu miaka kumi ipite hatachukuwa hatua za kujitoa kama ilivyo katika Ibara zilizopita atawajibika kubanwa na makubaliano haya kwa kipindi kingine cha miaka kumi na baada ya hapo anaweza kujitoa baada ya kila miaka kumi kupita kulingana na ibara hii.

#### **IBARA 40**

1. Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Kazi Duniani atotoa taarifa kwa wajumbe wote wa Shirika la Kazi Duniani juu ya kuandikishwa kwa maridhiano na kujitoa au kutofanywa kwake na wajumbe wa Shirika la Kazi Duniani.
2. Wakati akitoa taarifa kwa wajumbe juu ya kuandikishwa kwa maridhiano ya pili yaliyowasilishwa kwake, Mkrugenzi atawataarifu wajumbe siku ambayo makubaliano haya yataanza kufanya kazi.

#### **IBARA 41**

Mkurugenzi Mkuu atotoa taarifa kwa Katibu Mkuu wa Umoja wa Mataifa kwa ajili ya uandikishaji kulingana na Ibara ya 102 ya makubaliano ya Umoja wa mataifa, juu ya kuridhia au kujiondoa kwa wajumbe kwa kulingana na taratibu zilizopo katikaibara zilizotangulia.

#### **IBARA YA 42**

Kwa wakati ule kama itakapoonekana ni lazima, Chombo cha Utawala cha Ofisi ya Shirika la Makazi Duniani kitotoa taarifa ya utekelezaji kwenye MkutanoMkuu wa Umoja wa Mataifa wa Kazi na itachunguza mapendekezo ya kubadilisha au kupeleka agenda kwenye Mkutano Mkuu suala la kubadili au kurekebisha sehemu au makubaliano yote haya.

#### **IBARA YA 43**

1. Kama Mkutano utapitisha makubaliano mapya au kubadili sehemu ya makubaliano haya, basi vinginevyo kama sheria mpya itatamka:-
  - a). Maridhio ya wajumbe ya kubadili makubaliano haya yanapaswa kuruhusu wajumbe kutokuwa wajumbe mara baada ya mabadiliko bila kujali Ibara ya 39 ya sheria hii kama na wakati sheria hii inapaswa kuanza kufanya kazi.
  - b). Kuanzia siku hiyo makubaliano mapya itakapoanza kufanya kazi, makubaliano haya yataacha kuendelea kuridhiwa na wanachama.

2. Makubaliano haya kwa namna yoyote yataendelea kutumika kwa mfumo uliopo sasa hivi kwa wale wanachama ambao wameridhia makubaliano na ambao bado hawaridhia mabadiliko mapya ya makubaliano haya.

#### **IBARA YA 44**

Tafsiri ya Kiingereza na ya Kifaransa ya makubaliano haya yote yana msukumo na nguvu sawa kisheria.